


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI

MKOA WA MBEYA
Simu ya Mdomo: 252957440/252957447
Fax: 025-2590089/2590108
Baruazoteziandikwekwa
MkurugenziMtendaji (W) Mbarali



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 237,
RUJEWANA.

KITENGO CHA MANUNUZI.

Kitengo cha Manunuzi Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi Na. 07 ya mwaka 2011 kifungu cha 37.

Mfumo wa mawasiliano kwa mujibu wa sheria ni kuripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi, pia kitengo kina bajeti inayojitegemea ili kutekeleza majukumu yake.

MAJUKUMU YA KITENGO CHA MANUNUZI.

- 1) Kusimamia majukumu yote ya Manunuzi na Kuuza Mali za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali .
- 2) Kusaidia kazi za Bodi ya zabuni.
- 3) Kutekeleza Maamuzi ya Bodi ya Zabuni.
- 4) Kuandaa Mpango wa manunuzi wa Halmashauri na uuzaji wa Mali za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.
- 5) Kushauri Manunuzi ya Halmashauri na uuzaji wa Mali za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.
- 6) Kuandaa orodha ya mahitaji ya Idara na Vitengo.
- 7) Kuandaa Makabrasha ya Zabuni.
- 8) Kuandaa Matangazo ya Zabuni na Fursa Mbalimbali.
- 9) Kuandaa Mikataba mbalimbali ya manunuzi.
- 10) Kutoa makabrasha ya mikataba ambayo imepitishwa
- 11) Kutunza kumbukumbu mbalimbali za manunuzi na uuzaji wa mali za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.
- 12) Kuandaa orodha ya mikataba yote ambayo Halmashauri imeingia na wazabuni.
- 13) Kuandaa taarifa za mwezi, robo na mwaka za Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.
- 14) Kuandaa Taarifa za Robo na kuwasilishwa katika vikao vya Kamati ya Fedha Mipango na Utawala.
- 15) Kuratibu manunuzi na uuzaji mali za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.
- 16) Kuandaa Taarifa nyingine mbalimbali kadri zinavyohitajika na Mamlaka.